

Publication: Mwananchi

Country: Tanzania

Date: 27/05/2011

Dk Bilal: Sera mbovu, ukata vinaathiri ICT nchini

■ Fredy Azzah

MAKAMU wa Rais, Dk Mohamed Gharib Bilal, amesema Tanzania ni miongoni mwa nchi nyingi za bara la Afrika zinazokabiliwa na matatizo makubwa katika kuendeleza teknolojia ya habari na mawasiliano.

Dk Bilal aliyasema hayo juzi usiku, jijini Dar es Salaam, alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mwaka, kuhusu teknolojia hiyo.

Alisema matatizo sugu kuhusu sekta hiyo katika nchi za Afrika yanahusu sera, fedha, teknolojia duni, lugha, ukosefu wa wataalamu na maeneo mengi kutounganishwa katika mfumo wa mtandao.

"Kidogo hali inaanza kubadilika, ni jana tu (juzi), Rais Kikwete alizindua Windows 7, (programu ya kompyuta) ambayo itakuwa ikitumia lugha ya Kiswahili," alisema Dk Bilal.

"Tanzania imeshatambua umuhimu wa ICT katika kufikia malengo ya milenia, ndiyo maana imeingiza sera ya ICT katika dira ya maendeleo ya 2025," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Dk Bilal, asilimia 37 ya watu katika nchi za Afrika kwa sasa ni vijana wenye umri wa kufanya kazi, lakini asilimia 60 ya vijana hao hawana kazi.

Alisema hiyo inachangiwa na kasi ndogo ya ukuaji wa



Mwenyekiti wa mkutano mkuu wa sita wa kimataifa kuhusu Habari na Mawaliano katika Afrika, Theophilus Mlaki, akizungumza katika ufunguzi wa mkutano huo juzi usiku. Kushoto ni Makamu wa Rais Dk Mohamed Gharib Bilal. Picha na Fidelis Felix.

uchumi ambayo haitoi fursa ya kuajiri vijana wote.

Alisema ongezeko la wanafunzi, limesababisha kutokuwapo kwa uwiano wa ikama ya walimu lakini alieleza

matumaini yake kuwa tatizo hilo litamalizika hivi karibuni hasa ikizingatiwa vijana wengi sasa wanahitimu katika fani hiyo kila mwaka.

Mkufunzi wa Majeshi ya

Umoja wa Kujihami (Nato) Luteni Jenerali, Karilheinz Viereck, alisema ICT imekuwa msaada mkubwa katika kurahisisha utoaji wa mafunzo kwa majeshi hayo.

"Mtu unaweza kutumia mtandao kupata elimu kwa urahisi sana. Unapata elimu ambayo inaendana na mazingira uliyopo na unayoitaka," alisema Viereck.